



MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

Na.7. Msimu wa Kilimo 2022/23

Tathmini ya Novemba 21-30, 2022 na Matazamio kwa Kipindi cha Disemba 1- 10, 2022

MUHTASARI

- Wakulima wanashauriwa kuendelea kupanda mazao yanayokomaa mapema na kustahimili ukame
- Wakulima wanahimizwa kuzingatia utabiri wa hali ya hewa na kupata ushauri kutoka kwa maafisa ugani.

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2022

Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kupungua nguvu wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (Azore na Siberia) ikiendelea kuimarika kidogo. Hali hii iliendelea kuleta mchango katika kuusukuma ukanda mvua (ITCZ) kuelekea nchini kwetu hususan katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Viktoria pamoja na magharibi. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani lilionekana katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi wakati katika eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi joto la bahari lilikuwa la wastani hadi chini kidogo ya wastani.


Hali hii iliendelea kuleta mchango mdogo katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya mwambao wa pwani ya nchi hususan katika nusu ya pili ya dekadi.

Joto la bahari katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) lilikuwa la juu kidogo ya wastani na hivyo kutokuwa na mchango katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea magharibi mwa nchi.

TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2022

Katika kipindi hiki, maeneo mengi nchini yalipata mvua. Maeneo machache ya mkoa wa Tanga yalipata mvua nyingi zaidi ukilinganisha na maeneo mengine. Hata hivyo, baadhi ya maeneo katika mikoa ya Iringa, Mtwara, Lindi, Singida, Dodoma, Kilimanjaro na Arusha yalikuwa

makavu kama inavyoonekana kwenye Kielelezo.



Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Novemba 21-30, 2022

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2022

Mvua zilizonyesha katika dekadi hii zimeongeza unyevunyevu ambao umesaidia shughuli za kuandaa mashamba na kupanda mazao. Vilevile, ongezeko la unyevunyevu kwenye udongo katika baadhi ya maeneo yanayozunguka Ziwa Victoria lilisaidia katika ukuaji wa mazao yaliyopandwa hususan katika mkoa wa Kagera. Katika mkoa huo, mahindi yameanza kubeba hususan katika wilaya za Muleba na Bukoba. Maharage katika wilaya hizo yapo katika hatua za awali za kukomaa. Hata hivyo, hali ya mazao katika wilaya za Ngara na Biharamulo yaliathiriwa kutokana na vipindi virefu vya ukavu na mvua kuchelewa, ambapo baadhi ya wakulima walilazimika kurudia kupanda. Kwa maeneo ya mkoa wa Kigoma upandaji wa mahindi umeanza.

Maji na malisho kwa ajili ya mifugo na wanyamapori yameanza kupatikana kwa kiasi

kidogo katika maeneo machache kutokana na mvua zilizonyesha katika dekadhi hii.

HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2022

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito na mabonde mengi vimeanza kuongezeka kidogo hususan katika bonde la Ziwa Victoria kutokana na mvua zinazoendelea.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2022

Katika dikadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia katika kipindi hiki inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu wakati ile iliyopo katika kizio cha kaskazini inatarajiwa kuwa imeimarika kidogo. Hali hii inatarajiwa kuendelea kuusukuma ukanda mvua (ITCZ) kuelekea nchini kwetu hususani katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria pamoja na magharibi. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la magharibi ya bahari ya Hindi wakati katika eneo la mashariki ya bahari ya Hindi joto la bahari linatarajiwa kuwa la wastani. Hali hii inatarajiwa kutokua na mchango mkubwa katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya mwambao wa pwani ya nchi. Joto la bahari katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) linatarajiwa kuwa la juu kidogo ya wastani na hivyo kutokuwa na mchango katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea Magharibi mwa nchi yetu. Hata hivyo, kuimarika kwa wimbi anga (MJO) katika kipindi hichi kunatarajiwa kuwa na mchango katika kuimarisha utengenezaji wa mvua katika baadhi ya maeneo nchini.

HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2022

Maeneo ya kanda ya ya ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) na magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), Kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) na nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) inatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) inatarajiwa kuwa na vipindi vichache vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi hususan katika nusu ya pili ya dekadhi.

Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) inatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua katika maeneo machache hususan katika nusu ya pili ya dekadhi.

Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu na yenye vipindi vichache vya mvua nyepesi.

HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2022

Mvuua zinazotarajiwa zitaongeza unyevunyevu kwenye udongo ambao utasaidia ukuaji wa mazao yaliyopandwa.

Wakulima wanashauriwa kupanda mazao pale udongo utakapokuwa na unyevunyevu wa kutosha.

Wakulima na wafugaji wanashauriwa kuzingatia utabiri wa hali ya hewa na ushauri wa maafisa ugani kwenye maeneo yao.

Wavuvi wanashauriwa kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku ili kufanya maamuzi juu ya wakati sahihi wa kwenda kufanya shughuli za uvuvi.

Kwa ujumla inashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini.

HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2022

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuongeza kidogo hususan katika bonde la Ziwa Victoria. Hata hivyo, jamii inashauriwa kuvuna maji ya mvua kawa ajili ya matumizi ya baadae kwani hakuna ongezeko kubwa linalotarajiwa katika dikadi husika.